SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.23 NO. 1 2024
DOI: 10.51984/JOHS.V23I1.2904

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/johs

# KUCHUNGUZA UKOMBOZI ZINAZOJITOKEZA KATIKA RIWAYA YA "KULI"

*Ahmed Emhemad Badda, Ali Idris Ali Aburima

Department of Languages and African Studies, College of Languages, Sebha University, Libya

**Key words:**
Ukombozi
Riwaya ya Kuli
Jamii
Ukoloni
Uchomi

**ABSTRACT**
Makala hii inabainisha ukombozi uliojitokeza katika riwaya ya ( Kuli ), na kuelezea mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi katika kujenga dhamira ya ukombozi katika riwaya hiyo, na data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui, na upitiaji wa nyaraka. Data hizo zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na nadharia ya Saikolojia Changanuzi.

## دراسة ظاهرة الحث على التحرر الاجتماعي في رواية ( كولي **Kuli** ) للروائي شافي آدم شافي

*أحمد امحمد امبارك بده و علي إدريس علي أبوريمة

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
التحرر
رواية كولي
مجتمع
استعمار
اقتصاد

**الملخص**
ان هذه المقالة تدرس رواية "كولي " **Kuli** للروائي التنزاني " شافي أدم شافي"، وهدفها الأساسي توضيح ظاهرة التحرر الاجتماعي في الرواية والتي تحث الشعب التنزاني علي التحرر من الاستغلال، وأهمية التحرر في بناء الوطن، وأيضا توضح هذه المقالة الإستخدامات المختلفة للألفاظ في الوصف والتصوير، ومن خلال الدراسة توصل الباحث أن هناك تصورات عدة استخدمت في الرواية، وأن هناك ظاهرة سلبية سائدة في المجتمع التنزاني، ولوصول المجتمع للمواطنة والحقوق والواجبات والقيم الحديثة، يجب عليه التحرر الاجتماعي من الثقافات الخارجية لتحديث المجتمع وتطوره. وقد تم جمع وتحليل البيانات بإستخدام النظرية السيكولوجية الاجتماعية التي تساهم بشكل كبير في التغيير الاجتماعي في أنماط الحياة الاجتماعية ومسارها.

## Utangulizi

Ukombozi ni dhamira iliyotawala katika fasihi ya Kiswahili simulizi na andishi katika vipindi mbalimbali vya maendeleo ya jamii ya Waswahili na Watanzania kwa jumla (Mlacha, 1987). Jamii ya Waswahili imepata umaarufu mkubwa kutokana na harakati zake za kujikomboa kutoka katika mikono ya Wakoloni kwa lengo la kuleta usawa katika maisha ya wanaadamu (Adam, 2014). Mfano mzuri wa dhamira ya ukombozi unajitokeza katika mashairi mbalimbali ya Fumo Lingo yakiwa na Dhamira kuu ya kuhamasisha wananchi kuungana pamoja ili kujikomboa kutoka katika unyonyaji wa kikoloni (Mulokozi, 1996). Dhamira hii ya ukombozi haikuishia katika kazi za Fumo Liongo peke yake bali pia katika kazi za akina Muyaka bin Haji. Shaaban Robert, James Mbotela, Mathias Mnyampala, Euphrase Kezilahabi na Shafi Adam Shafi kuwataja kwa uchache tu. Kwa mfano, Shaaban Robert katika kazi zake za Kusadikika na Kufikirika ameelezea dhamira ya ukombozi kutoka katika unyonyaji wa kikoloni kwa mawanda mapana kwa kutumia ubunifu wa hali ya juu kabisa. Ubunifu huo ni ule wa mwandishi kutumia nchi inayoelea angani kuelezea madhila yanayofanywa na serikali ya kikoloni dhidi ya wananchi na kuwataka wananchi kuchukua hatua za kujikomboa.

Mwandishi Shafi Adam Shafi ameshughulishwa sana na dhamira ya ukombozi katika kazi zake za riwaya na huku riwaya yake ya Kuli ikiwa ni moja kati ya riwaya zake zilizoisawiri dhamira ya ukombozi kwa kina. Riwaya hii imejimbanua kama riwaya ya kiukombozi ambapo aina za ukombozi kama wa kifkra, kijamii, kiuchumi, kijinsia na kimasikini unajitokeza kwa kiasi kikubwa katika riwaya hii. Kabla hatujaanza kubainisha na kutoa maelezo ya kina kuhusu dhamira ya ukombozi katika riwaya ya Kuli ni vema tueleze kwa kujikumbusha maana ya ukombozi. Ukombozi ni hali ya kufanya jitihada na harakati za kujinasua kutoka katika hali ya unyonywaji, dhuluma, ufisadi na uonevu kwa kundi moja la watu kuwagandamiza kundi lingine kuelekea katika hali ya usawa (Mlacha, 1996). Mathalani, nchi za Ulaya zilitawala nchi mbalimbali duniani kimabavu na kunyonya rasilimali za mataifa hayo kwa kuwafanyisha

*Corresponding author.
E-mail addresses: Ahme.baddah@sebhau.edu.ly, (A. I. A. Aburima) Ali.aburima@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 21 December 2023 - Received in revised form 25 April 2024 - Accepted 05 May 2024*

kazi nyingi tena kwa malipo kidogo wananchi wan chi hizo zilizotawaliwa. Nchi za Afrika Tanzania ikiwemo nayo ilitawaliwa lakini baada ya muda kupita ilifanyika jitihada kubwa ya kujikomboa kutoka kwa wakoloni kwa njia mbalimbali. Hivyo basi, Shafi Adam Shafi kupitia riwaya yake ya Kuli amesawin vina dhamira mbalimbali za ukombozi.

**Lengo la utafiti**

Kuelezea mbinu za kisanaa, na aina za ukombozi zilizotumika katika riwaya ya ( Kuli ).

**Maswali ya utafiti**

1. Ni mbinu zipi za kisanaa zilizotumika katika kujenga dhamira ya ukombozi katika riwaya ya kuli ?
2. Ni aina gani za dhamira ya ukombozi zinazojitokeza katika riwaya ya kuli ?

**Dhamira ya Ukombozi wa Kifikra**

Ukombozi wa kifikra ni ile hali ya mtu kujitambua yeye ni nani hapo alipo ni wapi, yupo katika hali ipi kimaisha, zipi changamoto zinazomkabili, atumie mbinu zipi kutatua changamoto zinazomkabili, lini atatuwe changamoto hizo kwa kutumia rasilimali zipi. Nyerere (1967) anaeleza kuwa ukombozi wa kifikra ni kitu muhimu sana katika kufanikisha aina nyingine za ukombozi nazo kufanikiwa. Ikiwa mtu tayari ameshajikomboa kifikra ni rahisi sana kwa mtu huyo kujikomboa kielimu. Kijamii, kiuchumi, kisiasa na hata kutamaduni. Shafi Adam Shafi alilielewa sana suala hili ndio maana katika riwaya ya Kuli kunajitokeza dhamira za ukombozi. Kwa mfano, mwandishi anasema:

*"Mama." Rashid alianza, "mie najihisi nimeshakuwa mkubwa. Nahisi hivi sasa ni lazima nitafute kazi yoyote ile itakayoweza kuniendeshea maisha yangu nikusaidie na weye.*

*"Kazi gani utafanya weye mwanangu? Mie nilipokuambia nimetoka pwani weye ulihamaki bure na kupiga kelele. Sisi tupo wawili tu hapa. Tukisema taratibu tutasikiliza. Wewe kelele tu unafikin mie nimetoka pwani kukoga?" Rashidi aliendelea na maneno yake. "Mie nilikwenda pwani gatini kutafuta kibarua chochote kile lakini leo sikufanikiwa. Hata hivyo, nakwenda huko kila siku mpaka siku moja n'tapata kazi.*

*Rashid hakumweleza mama yake kitu chochote juu ya yote yaliyomtokea siku ile, aliondoka na kwenda kuteka maji mferejini akajaza mitungi ya jikoni na chooni na baada ya kwisha kukoga alikwenda jikoni pale alipoelekezwa na mama yake akachukua chakula chake akala (uk. 22).*

Katika dondoo hili tunaona dhamira ya ukombozi wa kifikra ikijitokeza kupitia maneno ya Rashid kwa mama yake. Maneno kama vile, "mie najihisi nimeshakuwa mkubwa, ni ushahidi tosha unaoonesha kuwa Rashidi ameanza kujikomboa kifikra. Hii ni kauli inayoonesha kuwa kijana huyu Rashid tayari ameshajitambua yeye ni nani na anatakiwa kufanya nini ili aweze kuendesha maisha yake pamoja na yale ya familia yake yaani kumsaidia mama yake ambaye tayari ameshakuwa mtu mzima (yaani mzee anayehitaji kusaidiwa na mwanae), Freud (1896) anaeleza kuwa mtoto anapoanza kuwa na fikra za kujitegemea ni hatua kubwa sana katika makuzi yake inayoonesha kuwa tayari anaweza kubeba na kutimiza majukumu mbalimbali katika maisha yake na familia yake. Kinyume chake, mtoto anayefikisha umri wa kujitegemea na bado hawezi kujitegemea ni uthibitisho kuwa kijana huyo bado hajajikomboa. Mfano wa Rashidi ni mzuri sana na unapaswa kuigwa na vijana katika jamii ya leo ili kuendeleza dhana ya uwajibikaji na kufanya kazi katika jamii.

Katika dondoo hilo hapo juu, mwandishi anatuonesha kuwa ukombozi wa kifikra humwezesha mtu kutochagua kazi ya kufanya ili kujipatia kipato. Kazi yoyote ile ya halali iwe nzuri au mbaya kwa mtazamo wa watu huifanya bila ya kujali watu watasema nini. Mama yake Rashid alipata wasiwasi kama mwanae atamudu kufanya kazi ya ukuli bandarini kutokana na umri wake kuwa bado ni mdogo. Maneno ya mama yake kuwa, "kazi gani utafanya weye mwanangu," ni ishara ya kuonesha kuwa Rashid alikuwa bado mdogo kumudu kazi ya ukuli bandarini. Kauli hii inaonesha huruma aliyonayo mama kwa mtoto wake. Lakini huruma hii haisaidii kwani tayari baba wa mtoto mbaye ni Majaliwa ameshafariki na mama ni mtu mzima asiyeweza tena kufanya kazi na anahitaji kusaidiwa. Hivyo, Rashidi ni lazima afanye
Kazi ili aweze kuendesha maisha na tena hana uhuru wa kuchagua kazi kutokana na hali halisi ya mambo ilivyo kwa wakati huo.

Sambamba na hilo, dondoo lililopo hapo juu linaonesha kuwa Rashidi ni mtu ambaye tayari alikwishapata ukombozi wa kifikra ndio maana hakumweleza mama yake masaibu yaliyomkuta akiwa katika harakati za kutafuta kazi bandarini. Rashidi alifahamu fika kuwa akimweleza mama yake masaibu yaliyomkuta bandarini atamfanya aumie zaidi na kisha kumzuia mwanae asiende tena gatini kutafuta kazi. Maneno. "Rashid hakumweleza mama yake kitu chochote juu ya yote yaliyomtokea siku ile..." yanaonesha kuwa Rashidi ni mtu alikuwa tayari ameshajikomboa kifikra. Katika hali ya kawaida, mama ni mtu anayeumia sana pale anaposikia mtoto wake amepatwa na tatizo fulani. Ukombozi huu wa kifikra aliokuwa nao Rashidi I mfano wa kuigwa na vijana wengine wote hususani katika kutumia busara na hekima wanapoongea na wazazi wao ili kutosababisha matatizo. Mama yake Rashidi alikuwa ni mgonjwa na pengine kama angepata kufahamu yale yaliyomkumba mwanawe ugonjwa wake ungezidi mara dufu.

Ukombozi wa kifikra katika riwaya ya Kuli unajitokeza tena katika kurasa mbalimbali za riwaya hii lengo likiwa ni lilelile la umuhimu wa watu kujitambua kuwa wao ni nani na wanamajukumu gani katika jamii. Mwanadishi anasema:

*Rashidi alifanya kazi hiyo pamoja na akina Mzee Tindo kwa siku nyingi na siku zilivyopita alizidi kuona ugumu wa kazi waliyokuwa wakifanya. Alibaini kwamba malipo waliyokuwa wakipata hayakulingana hata kidogo na kazi waliyoifanya.*

*Kwa muda mrefu hakujua afanye nini ili awajulishe wenzake hayo mawazo yake. Na isitoshe aliogopa kwamba huenda wenzake*
*Wasimwelewe na badala yake wakamchonganisha na kumshitaki kwa*

*Tajiri wao akapoteza kazi na kutia maisha yake mashakani. Mwisho*

*Aliamua kuwadokeza wenzake lakini kwanza kama wazo lililomponyoka tu lisilo na kiini. "Mnajua nyie?" Rashidi alianza wakati walipokwisha kugawana pesa.*

*"Mie nahisi hawa matajiri tunawafanyia kazi wanapata faida kubwa*

*Na sisi wanatulipa pesa kidogo kwelikweli." Hakuna hata mmoja katika wenzake Rashidi aliyeweza kufikiri kwamba Rashidi angethubutu kusema maneno kama yale. "Weye umewahi kupata pesa kama unazopata hapa katika maisha yako?" Mzee Tindo alimuuliza Rashidi huku akimkunjia, uso akionyesha hamaki.*

*"Kweli sikuwahi kupata pesa nyingi kama nionazopata hapa lakini vilevile, sikuwahi kufanya kazi ngumu kama kazi hii tunayofanya sisi," Rashidi alijibu kwa sauti ndogo huku kainama chini akiwa hawezi kumtazama Mzee Tindo usoni (uk.44).*

Mwandishi anatuonesha kuwa Rashidi ni mtu ambaye tayari alikwisha jikomboa kifikra na kutumia fikira zake kuwasiaidia wafanyakazi wenzake katika kudai haki zao. Ukombozi huu wa kifikra unajitokeza pale ambapo Rashidi ameweza kutambua kuwa malipo wanayopewa ni kidogo sana ikilinganishwa na kazi ngumu wanayoifanya. Maneno kama "mie nahisi hawa matajiri tunawafanyia kazi wanapata faida kubwa na sisi wanatulipa pesa kidogo kwelikweli," ni uthibitisho wa kwamba ukombozi wa kifikra unajitokeza katika riwaya ya Kuli. Itakumbukwa kuwa Rashidi ni mtu ambaye alitoka katika familia masikini isiyokuwa hata na uwezo wa kupata mlo mmoja na mwenye nyumba tayari alikwisha anza kuwadai kodi ya nyumba tena kwa kishindo.

Hivyo, kupata malipo ya shillingi 3 kwa siku ilikuwa ni fedha nyingi sana kumsaidia katika kuendeshea maisha yake vizuri. Hili lingemfanya anyamaze kimya na asiwe mtu wa kuzungumzazungumza kwamba malipo wanayolipwa ni kidogo
Ikilinganishwa na kazi wanayofanya. Hata hivyo, saikolojia ya Rashidi tayari ilikwishakomboka kifikra ndio maana hakujali kuwa na mawazo kama haya kuhusiana na malipo wanayolipwa kwa kutwa huko bandarini. Hili linathibitishwa na maneno yaliyopo katika aya ya mwisho ya dondoo lililopo hapo juu kuwa, "kweli sikuwahi kupata pesa nyingi kama ninazopata hapa lakini vilevile sikuwahi kufanya kazi ngumu kama hii tunaifanya sisi." Hii ni kauli inayoonesha dhamira ya ukombozi wa kifikra ikijitokeza katika jamii na inapaswa kila mwanajamii awe na tabia na fikira kama hizi za Rashidi ili kuleta ukombozi wa kweli katika jamii.

Kuogopa kusema ukweli kwa sababu ya kuhofia kufukuzwa kazi ni jambo ambalo linaonesha kuwa ukombozi wa kifikra bado haujadhihiri kutoka kwa wanadamu walio wengi. Wafanyakazi wenzake na Rashidi kama Farjalla na wengine walikuwa waoga kueleza ukweli wakihofia kupoteza kazi. Hali haikuwa hivyo kwa Rashidi kwani ingawa hata yeye alikuwa na uoga fulani lakini alithubutu kueleza kweli kutoka moyoni mwake. Kitendo cha kuthubutu kusema ukweli bila ya kujali matokeo yake knaonesha kuwa Rashidi alikomboka kifikra na alitaka wafanyakazi wenzake nao waige mfano wake na wawe kama yeye. Kitendo cha kufanyishwa kazi nyingi tena ngumu kwa malipo kidogo ni kitendo cha kinyonyaji na dhuluma dhidi ya wananchi na hakitakiwi kuvumiliwa hata kidogo (Shivji, 2002; Mlacha, 1991; Khamis, 2007).

Baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusiana na dhamira ya ukombozi wa kifikkra katika riwaya ya Kuli sasa itakuwa ni vema tutazame dhamira ya ukombozi wa kijamii kama inavyojitokeza katika riwaya hiyo.

**Dhamira ya Ukombozi wa Kijamii**

Jamii ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu katika maisha yake ya kila siku na kutokana na vitu hivyo ndipo mwanadamu anaweza kutimiza majukumu na wajibu wake wa kila siku (Madumulla, 2009). Vilevile, tunaweza kusema kuwa jamii ni kundi la watu wanaoishi katika eneo fulani la kijiografia wakiwa na makazi yao, uongozi wao, elimu yao, huduma zao za afya, ardhi yao, shughuli zao za uzalishaji mali, shughuli za kiutamaduni na kidini katika makazi yao rasmi (Muhando na Balisidya, 1976). Hivyo, tunaposema juu ya ukombozi wa kijamii tunamaana kuwa wanajamii wanaweza kufanya shughuli zao za kijamii na kupata huduma za kijamii bila vipingamizi vya kibaguzi vya aina yoyote ile. Kwa mfano, katika kipindi cha ukoloni wananchi wengi wa nchi za Kiafrika Tanzania ikiwemo walinyimwa kupata huduma nzuri za elimu, afya, makazi, maji, barabara na kuwekwa katika tabaka la chini. Wazungu, Wahindi na Waarabu ndio waliokuwa katika tabaka la juu na kati mutawalia na kujipatia huduma bora za kijamii. Baada ya kupatikana kwa uhuru juhudi mbalimbali zilifanyika katika kuhakikisha kuwa ukombozi wa kijamii unafanyika ili kuweza kuwapatia wananchi huduma bora za kijamii (Nyerere, 1977).

Shafi Adam Shafi hayuko nyuma katika kusawiri dhamira ya ukombozi wa kijamii akiamini kuwa ili jamii yoyote ile duniani iweze kupata maendeleo ni lazima jamii hiyo iwe imeweza kuwapatia watu wake huduma bora za kijamii ikiwemo ile ya afya. Akithibitisha ukweli huu mwandishi anasema:

*Aaaaa! Akaanguka huku akipiga kelele nyingi kwa maumivu. Wafanyakazi wenzake na wengine waliokuwa karibu walimzunguka huku wakijaribu kumsaidia mfanyakazi mwenzao aliyekuwa akipiga*
*Mikambe kama mtu aliyekata roho. Palepale alikwenda kuitwa mkuu wa gati ambaye alikuwa Mwingireza. Muda si muda alifika pale alipo majeruhi yule. Alimbonyezabonyeza na kumfanya yule mfanyakazi azidi kupiga kelele kwa maumivu na mara yule mzungu akasema, "sasa peleka yeye nyumbani."*

*"Tumpeleke nyumbani?" Akida aliuliza. "Lazima tumpeleke*

*Hospitali, ameumia sana huyu," aliendelea. "Nani tapeleka yeye hospitali?" Yule Mzungu aliuliza. "Gari la kampuni si lipo?" Wote waliopo pale walisema kwa umoja wao. Yule Mzungu ambaye alikuwa amechutama huku akimgeuzageuza majeruhi yule alisimama na kuwatazama wafanyakazi wale mmojammoja na kwa ukali alisema, "Ninyi hapana jua gari ya kampuni iko kazi mingi?"*

*"Muhimu hiyo kazi au huyu mtu aliyeumia? Unafikiri kazi ni muhimu kuliko maisha ya mtu?" Akida aliuliza kwa hamaki. "Hiyo hapana shauri yangu," alijibu yule Mzungu na bila ya kumtazama yeyote katika watu wale waliokuwapo pale alikwenda zake.*

*Makuli wote walipigwa na mshangao, hawakujua la kufanya; mwenzao amelala chini mahututi, kauli hana, amebakia kuugua tu kwa maumivu makubwa aliyokuwa nayo.*

*"Mie n'na shauri moja," Majaliwa alisema kwa ghafla, "tuchangeni, na pesa zitakazopatiana tutakodi gari tumpeleke hospitali (uk. 06).*

Dondoo hili linaonesha namna wakoloni walivyokuwa hawawathamini wanyakazi wao wenye asili ya Kiafrika kwa kuwatumikisha kwa malipo kidogo na wanapopata matatizo au ajili kazini hawapatiwi matibabu. Katika dondoo hili tunaoneshwa kuwa mmoja kati ya makuli alipata ajali ya kuumizwa na mzigo mzito waliokuwa wameubeba lakini bosi wao hakutaka apelekwe hospitali na badala yake aliwataka makuli wenzake wampeleke nyumbani. Hili linabainika pale asemapo, "mzungu akasema, sasa peleka yeye nyumbani," akimaanisha kuwa kuli yule hana faida tena na sasa apelekwe

nyumbani. Huu bila shaka ni uonevu na unyonyaji wa hali ya juu sana usiokuwa na mfano wa kupigiwa kwani umekosa hata chembe ya ubinadamu. Hii ndio ilikuwa tabia ya wakoloni katika sekta mbalimbali walizoanzisha katika

Makoloni yao ambapo walimuona mfanyakazi kuwa na umuhimu kwao pale tu ambapo ana afya nzuri ya kufanya kazi. Inapotokea mfanyakazai amepata maradhi au ajali ambayo itasababisha afya yake kuzorota huonekana hana thamani tena kwa bosi wake.

Hata hivyo, makuli wote wakiongozwa na Akida na Majaliwa hawakukubaliana hata kidogo na maelekezo ya bosi wao la kumpeleka muathirika wa ajali hiyo nyumbani na walionesha kwamba muathirika huyo lazima apelekwe hospitali na siyo nyumbani. Hili linabainika pale mwandishi asemapo, "lazima tumpeleke hospitali, ameumia sana huyu," kauli iliyotolewa na Akida mmoja kati ya makuli wa kundi la akina Majaliwa. Kauli hii kwa hakika inaonesha kuwa kuwa makuli walidhamiria kuleta ukombozi wa kjamii ambapo watu wote walistahili kupatiwa huduma za afya bila ubaguzi wa rangi, jinsia, dini wala kabila. Kauli kama hii kutolewa mbele ya Mzungu aliyeendekeza ubaguzi wa rangi ni hatua muhimu sana katika kuleta ukombozi wa kweli wa kijamii kwa wananchi wote wa Afrika na wale wa Tanzania wakiwepo.

Kimsingi, huduma za afya ni moja kati ya huduma za kijamii ambazo ni za muhimu sana katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi na watu wote katika jamii wanakuwa na afya njema ili waweze kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ufanisi na tija. Ni jambo la kushangaza sana kumuona kiongozi au mkuu wa kazi asiyejali afya za wafanyakazi wake kwa kuwa haelewi kuwa mtumishi asiye na afya njema hawezi kufanya kazi vizuri na kuiletea kampuni au shirika faida ya kutosha. Bila shaka kiongozi makini anajua umuhimu wa wafanyakazi wake kuwa na afya njema lakini

Ubaguzi wa rangi na unyonyaji dhidi ya watu wengine unaweza kumfanya kiongozi kama huyo mzungu wa bandarini kutokuwapatia tiba wafanyakazi wake tena wale waliopata ajali wakiwa kazini. Mwandishi anatuonesha kuwa makuli wakiongozwa na Majaliwa walikubaliana kuchanga fedha ili zitumike katika kumpatia matibabu kuli mwenzao aliyeumia kazini. Majaliwa alitoa kauli kuwa, "mie n'na shauri moja, "Majaliwa alisema kwa ghafla, "tuchangeni, na pesa zitakazopatikana tutakodi gari tumpeleke hospitali." Hii ni kauli ninayoonesha kuwa jamii iko tayari katika kuleta ukombozi wa kweli wa huduma za kijamii ambapo wanaweza kuchangiana ili kupata fedha za matibabu.

Dhamira ya ukombozi wa kijamii inaendelea kujitokeza katika riwaya ya Kuli kwa mwandishi kutuonesha kuwa elimu ina nafasi kubwa sana katika kumpatia maendendeleo mtu mmojammoja na jamii kwa jumla. Elimu ni moja kati ya masuala ya kijamii ambapo mwanajamii yeyote akishapata elimu tayari amekomboka kijamii na anaweza pia kuikomboa jamii yake katika masuala mbalimbali yakiwepo ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Mhusika Rashidi katika riwaya ya Kuli alilijua sana suala hili na ndio maana aliamua kwenda kujifunza kusoma na kuandika ili iweze kumsaidia katika kujiletea ukombozi wa kweli katika jamii. Mwandishi anasema:

*Siku ile ilikuwa ni siku ya mgeuko mkubwa katika maisha ya Rashidi. Hakufikiria katika maisha yake kama angekuwa na azma ya kusoma. Kabla ya kuja hapo Rashidi alifikiri umri wake haukumruhusu tena kusoma lakini alipata moyo mkubwa alipoona kwamba baadhi ya wanafunzi wenzake walikuwa watu wazima walioweza kumzaa. Hivyo akawa anawaza, "Ama maneno ya faraji ni kweli tupu. Aliniambia kwamba kuna watu wazima wanaoweza kunizaa na hata kunijukuu ambao wanasoma." Hata hive alijiuliza kama huku*

*Kusoma kungelimsaidia chochote katika maisha yake kwani aliona kazi yake haikuhitaji kisomo.*

*"Lakini nafikiri kuna umuhimu wa kujua kusoma na kuandika mana'ake zile karatasi anazozigawa faraji bandarini lazima niweze kuzisoma mwenyewe, "alijisemea tena na kuendelea, "Mpaka lini nitamtumainia Faki kunisomea?"*

*Jambo la kwanza alilolifanya siku ya pili alipokuwa anarejea nyumbani ilikuwa kupitia darajani na kununua kalamu na kitabu. Alipofika nyumbani alikoga na kubadilisha nguo akaingia chumbani kwa mama yake na kumjulia hali. Alimpa pesa za matumizi ya siku ya pili na baada ya hapo alitia kalamu yake mfukoni na kitabu mkononi mpaka michenzani (uk.74).*

Katika dondoo hili tunaoneshwa dhamira ya ukombozi wa kijamii kwamba kila mtu akiwa na fursa sawa ya kupata elimu inawezekana bila kujali umri wa mtu. Mhusika Rashidi anaonekana kuamini kuwa elimu atakayoipata itamsadia katika kujitegemea katika kufanya masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusoma barua na maelekezo yote ya kazi atakayokuwa akipewa na mkuu wake wa kazi. Hii itamsaidia kuepukana na adha ya kuomba kusomewa kila kitu na rafiki zake jambo ambalo hata wakati mwingine siri zake zinaweza kufahamika kwa watu wengine. Rashidi alionekana kutaka kukata tamaa kuwa yeye ni mtu mzima sasa na hivyo hatoweza kusoma kwani wanaotakiwa kusoma ni watoto wadogo. Hata hivyo, alikata shauri na kuamua kusoma jambo ambalo baada ya kukuta katika darasa kuna watu ambao wanastahili kuwa wazazi wake na wengine babu na bibi zake nao wanasoma.

Kimsingi, elimu ni kitu muhimu sana katika maisha ya jamii kwani kutokana na elimu ndipo ukombozi wa kweli kwa wanajamii unaweza kupatikana. Ikiwa mtu atakuwa amepata elimu nzuri itamsaidia katika kufanya mambo yake kitaalamu zaidi na pia mtu huyo ataweza kuwasaidia watu wengine kujikwamua kimaisha. Vilevile, aina nyingine za ukombozi kama vile ukombozi wa kiuchumi, kiutamaduni, kijinsia

Na kifikra unaweza kufanikiwa kwa ufanisi zaidi pale mwanaukombozi anapokuwa tayari amekomboka kielimu. Hivyo, tunashauri jamii na serikali kuhakikisha kuwa elimu inatolewa kwa watu wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote ile ili baadae taifa liwe na watu wanaojitambua, wanaojali wengine, wenye heshima, unyenyekevu na wawajibikaji kwa ajili ya maendeleo ya taifa zima.

Baada ya kueleza kwa mapana juu ya ukombozi wa kijamii na kuonesha kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha na jambo la muhimu kuwa kila mwanajamii kuwa na elimu, ni vyema sasa tutazame dhamira ya ukombozi wa kijinsia kama inavyojitokeza katika riwaya ya Kuli.

**Ukombozi wa Kijinsia**

Ukombozi wa kijinsia ni moja kati ya masuala yanayozungumziwa sana katika kipindi hiki cha karne ya ishirini na moja na asili yake hasa ikiwa ni katika karne ya kumi na tisa. Ukombozi wa kijinsia unatokana na mawazo ya Wanaufeministi wanaoamini kuwa mfumo dume uliopo katika jamii unachangia kwa kiasi kikubwa

kunyanyapaa mwanamke na kumfanya asipate haki sawa na mwanaume (Koda, 2000). Ngaiza (2002) kwa mfano, anaeleza kuwa mfumo dume katika jamii umemfanya mwanamke kuwa ni kiumbe wa ndani anayestahili kushughulikia masuala ya kupika chakula, kufua nguo, kuosha vyombo, kusafisha nyumba, kulea watoto, kumlea mume, kuwalea wazazi wa mume pamoja na ndugu zake (ndugu wa mume). Kutokana na kufanya kazi hizi mwanamke amenyimwa fursa ya kupata elimu, kufanya kazi za uzalishaji mali kwa umiliki wake binafsi, kunyimwa haki ya kuwa kiongozi na pia kunyimwa haki ya kurithi mali (Ramadhan, 2013).

Kutokana na hali hii ndipo sasa likaibuka kundi la wanaufeministi ambao wamekuwa wakidai kumkomboa mwanamke ili naye aweze kupata haki na fursa sawa kama vile anavypata mwanaume. Mwandishi Shafi Adam Shafi ameisawiri vizuri dhamira hii ya ukombozi wa mwanamke katika riwaya ya Kuli pale alipotuonesha kuwa mwanamke si kiumbe wa kukaa kimya tu hata kama anaonewa bali anatakiwa kuwa jasiri katika kutetea haki yake. Mwandishi anasema:

*Bi Mashavu alikuwa ni mwanamke msemaji sana na kwa sababu ndogo tu aliweza kupiga kelele kutwa. Alikuwa anaweza kumwambia mtu jambo lolote bila ya kujali, na kwa jeuri; wanawake wachache sana katika mtaa wa Gulioni waliweza kushindana naye (uk.21).*

Dondoo hili linaonesha kuwa katika jamii ya Waswahili wa pwani mwanamke ni kiumbe ambaye hakuwa na ruhusa ya kusema chochote cha kupinga au kukemea jambo ambalo linafanywa na mwanaume kinyume na matarajio ya mwanamke. Hii ni kutokana na mafundisho ya dini ya Kiislamu ambapo mwanamke alipaswa kumheshimu sana mumewe na asithubutu kusema chochote hata kama ni kibaya kwake hicho anachofanyiwa. Hili linabainika pale mwandishi anaposema, "wanawake wachache sana katika mtaa wa Gulioni waliweza kushindana naye." Hii ina maana kuwa wanawake wengi wa jamii hiyo ni watu ambao hawakuwa na uhuru wa kusema na kujieleza kama alivyoweza kufanya Bi Mashavu. Kwa mujibu wa Koda (2000) kitendo cha mwanamke kuwa na ujasiri wa kuzungumza au kusema jambo ambalo linamkera mbele ya mwanaume ambaye anamkera ni ukombozi tosha kwa jinsia ya kike. Tunasema ni ukombozi kwa sababu wapo baadhi ya wanawake ambao wanafanyiwa vitendo vya kikatili lakini wanaogopa kusema na hatimaye kupata madhara makubwa ya kiafya na kisaikolojia.

Katika dondoo la hapo juu mwandishi anaonesha kuwa Bi Mashavu hakuwa mtu muoga bali aliweza kumwambia mtu yeyote jambo lolote bila ya aibu. Mwandishi anasema, "alikuwa anaweza kumwambia mtu jambo lolote bila kujali na kwa jeuri," akiwa na maana kuwa Bi Mashavu ni mtu ambaye ana uhuru wa kusema kile ambacho anaamini kuwa ni sahihi kukisema au kukipinga. Huu ni mfano mzuri ambao ukiigwa na wanawake unaweza kuleta ukombozi mkubwa kwa jinsia ya kike. Hata hivyo, haina maana kuwa mwanamke anao uhuru wa kuzungumza mambo tu bila ya kuwa na kipimo bali anapaswa kutazama lipi ni jambo baya linapaswa kukemewa na lipi ni zuri linapaswa kuenziwa na kutunzwa. Kwa kuzingatia kanuni hii, ukombozi kamili wa mwanamke utafanikiwa na mfumo dume utapungua kwa kiasi kikubwa kama si kwisha kabisa.

Dhamira ya ukombozi wa mwanamke inajitokeza tena pale ambapo mke wa Rashidi aliyefahamika kwa jina la Amina alipokuwa akimuuliza mumewe sababu za kuchelewa kurudi nyumbani kila mara. Mwandishi anasema:

"Leo umezidi tena!" Amina alianza kusema, tokea saa uliyotoka kazini mpaka sasa hivi! Ulikuwa wapi!

*Rashidi hakujibu kitu, alinyamaza kimya na kuingia chumbani. Lakini kunyamaza kimya kwake hakukumsaidia kitu kwani Amina alimfuata hukohuko chumbani huku akiendelea na malalamiko yake, "mimi nasema na wewe, wewe unanifanya kama mwendawazimu ndiyo?" Rashidi aligeuka nyuma na kumtazama Amina aliyekuwa amesimama mlangoni. Alitabasamu na kutaka kusema kitu lakini kabla hajawahi kusema Amina aliingilia kati, "unacheka nini? Unafikiri hayo unayoyafanya mazuri? Toka ulipotoka kazini Magharibi mpaka sasa hivi, mwenzako nimo ndani ya nyumba peke yangu wewe basi unatokomea huko na starehe zako, "Amina alisema huku midomo inamtetemeka kwa hamaki (uk. 151).*

Katika dondoo hili mwanadishi anaonesha namna Amina alivyokuwa na ujasiri wa
Kumuuliza mumewe sababu za kuchelewa kurudi nyumbani mara baada ya kutoka kazini. Katika jamii ya Waswahili ni mwanamke tu ndiye anayetakiwa kuomba ruhusa na kutoa udhuru kwa mumewe kuwa anakwenda mahali fulani na atachelewa kurudi nyumbani. Mwanaume yeye kwa upande wake ni kiongozi wa nyumba na anaweza kufanya jambo lolote lile bila ya kumtaka ruhusa au udhuru mkewe. Hivi ndiyo ilivyokuwa kwa Rashidi ambaye aliamua kuchelewa kurudi nyumbani na siku nyingine asirudi kabisa bila ya kutoa taarifa. Kutokana na hali hiyo halikuwa jambo la kawaida kwa mwanamke kumuuliza mumewe sababu za kuchelewa kurudi nyumbani. Hata hivyo, Amina ameonesha ujasiri mkubwa bila kuogopa akimtaka mumewe amueleze ni kwa nini alichelewa kurudi nyumbani na alikuwa akifanya nini huko alipokuwa. Hii bila shaka inaonesha kuwa ukombozi wa mwanamke katika kutaka fursa sawa na kuheshimiwa unadhihiri katika jamii ya Tanzania na duniani kote kwa jumla. Hata hivyo, mabadiliko hayo ni ya taratibu lakini inaonekana kuwa siku moja mambo yatafanikiwa vizuri zaidi (Mwaipopo, 1990).

Baada ya kueleza kwa kina juu ya dhamira ya ukombozi wa kijinsia kama inavyojitokeza katika riwaya ya Kuli ni vema sasa tutazame dhamira ya ukombozi wa kiuchumi katika riwaya hii ya mwandishi Shafi Adam Shafi.

**Ukombozi wa Kiuchumi**

Ukombozi wa kiuchumi ni dhamira inayojitokeza sana katika kazi mbali za fasihi ikiwemo riwaya ya Kuli ya Shafi Adam Shafi. Ukombozi wa kiuchumi ni ile hali ya wananchi kuweza kufanya shughuli za uzalishaji mali kwa manufaa yao binafsi na taifa lao pia. Sambamba na hilo, ukombozi wa kiuchumi pia unahusu haki ya
Wananchi kumiliki nyenzo za uzalishaji mali kama vile ardhi, mitaji, zana za kufanyia kazi na elimu ya ujasiriamali. Dhamira ya ukombozi wa kiuchumi imejitokeza sana katika kazi za fasihi simulizi na andishi kutokana na ukweli kuwa wakoloni waliotawala katika nchi za Afrika Tanzania ikiwa ni mojawapo walinyonya rasilimali za taifa kwa manufaa yao wenyewe. Wananchi walinyang'anywa ardhi yao, wakalazimishwa kufanya kazi ngumu kwa malipo kidogo na kisha wakalipishwa kodi kubwa kwa manufaa ya serikali ya kikoloni na si manufaa ya wananchi.

Kimsingi, kutokana na hali ya unyonyaji wa kiuchumi uliokuwa ukifanywa na wakoloni ndio maana kazi mbalimbali za fasihi kama Kuli zikatungwa kusawiri hali

hii. Kutokana na hali ya wakoloni kuwanyima wananchi wengi ajira nzuri zenye malipo mazuri baadhi yao walilazimika kujiajiri wao wenyewe ili kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yao. Miongoni mwao alikuwa ni Bi Mshavu aliyelazimika kufanya biashara ndogondogo mara baada ya mumewe aliyekuwa akifanya kazi ya ukuli bandarini kufariki. Majaliwa ambaye ni mume wa Bi Mashavu alifariki dunia kutokana na kuendelea kufanya kazi ngumu ya ukuli licha ya umri wake kuwa mkubwa na hivyo kupata ugonjwa wa kiharusi. Kufa kwa Majaliwa ilikuwa ni mtihani mkubwa kwa familia yake kwani yeye ndiye aliyetegemewa kwa kila kitu cha kuendeshea maisha ya familia yake. Mwandishi anasema:

*Baada ya kifo cha Majaliwa. Bi Mashavu ilimbidi afanye kazi ili aweze kuendesha maisha yeye na mtoto wake Rashidi ambaye sasa alikuwa mkubwa. Hakuna kazi aliyoweza kuifanya isipokuwa kazi ya biashara ndogondogo kama vile kupika maandazi, kupika mboga na biashara nyingine kama hiyo. Rashidi alimsaidia mama yake katika kazi zake zote; siku nyingine alitembeza mikate ya kusukuma au maandazi na siku nyingine alitembeza mihogo ya kuchemshwa.*
*Rashidi hakuweza kuishi katika hali hii na baada ya kufikiri sana aliona bora atafute kazi ya kuweza kumsaidia yeye pamoja na mama yake Bi Mashavu. Kazi ya kwanza aliyofikiria ilikuwa ni kazi ya marehemu baba yake, kazi ya ukuli (uk.08).*

Kimsingi, katika dondoo hili kunaoneshwa namna Bi Mashavu na mwanawe Rashidi walivyoamua kujikomboa kiuchumi mara baada ya kifo cha Majaliwa. Kitendo cha Bi Mashavu kuamua kufanya biashara ya kuuza maandazi, mikate na mihogo ni ishara ya ukombozi wa kiuchumi ambao utawawezesha kupata mahitaji yao ya kila siku katika maisha. Huu ulikuwa ni uamuzi mzuri na sahihi kwani baada ya kifo cha Majaliwa Bi Mashavu hakuwa na mtu mwingine yeyote ambaye angeweza kumsaidia kupata mahitaji ya kila siku. Hii inaonesha kuwa Bi Mashavu alikuwa ni mama mbunifu aliyejali familia yake ndio maana aliamua kufanya biashara ndogondogo ili kupata kipato cha kujikimu. Huu ni mfano mzuri wa mwanamke ambaye amejikomboa si kifikra tu bali pia kiuchumi na inafaa wanawake wote katika jamii kuiga mfano huu mzuri.

Kimsingi, katika jamii ya leo wapo wanawake wengi sana ambao wanajishughulisha katika shughuli za ujasiriamali kwa kufungua biashara ndogondogo za kujipatia kipato. Hii imewafanya wanawake kuondokana na utegemezi wa kila kitu kutoka kwa mwanaume na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa unyanyasaji wa kijinsia (Koda, 2000). Mwanamke wa leo anao uwezo wa kumsaidia mumewe majukumu ya kulipa ada za shule za watoto wao na pia kununua mahitaji mbalimbali ya nyumbani.

Katika miaka ya hapo nyuma majukumu haya yalifanywa na mwanaume peke yake na wakati mwingine alielemewa na kushindwa kuyatimiza kwa ukamilifu. Huu ni
Mfano mzuri ambao tunapendekeza uweze kuigwa na wanajamii kwa ujumla wao kwa kuwa utasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa jamii.

Dhamira ya ukombozi wa kiuchumi inaendelea kujitokeza zaidi katika aya ya mwisho ya dondoo lililopo hapo juu ambapo tunamuona Rashidi naye akiamua kutafuta kazi ya ukuli ili aweze kupata kipato. Mawazo ya Rashidi katika dondoo hilo yanaonesha kuwa tayari ameshakuwa mtu mzima na saikolojia yake inamwelekeza kwamba sasa anatakiwa kufanya kazi ili kuweza kujisaidia yeye mwenyewe pamoja na mama yake. Huu ni mfano mzuri wa kijana kuwa na mawazo kama haya na inapasa vijana wote katika jamii kuiga mfano huu. Rashidi anaonekana kuwa si mtu mbinafsi mwenye kujijali yeye mwenyewe lakini anamjali mama yake pia.

Katika maisha ya siku hizi ni vijana wachache sana ambao wana fikira na mawazo kama ya Rashidi. Wengi wao wanaonekana kuwa ni wabinafsi na hufikiria matumbo yao na mambo ya starehe kwa manufaa yao wenyewe. Bila shaka, kijana wa aina hii bado hajakomboka si kifikra tu bali hata kiuchumi. Kijana aliyekomboka kiuchumi ni yule ambaye anafanya kazi kwa juhudi na maarifa lakini pia hachagui aina ya kazi na kukataa baadhi ya kazi.

Baada ya kutoa maelezo ya kina kuhusiana na dhamira ya ukombozi wa kiuchumi katika riwaya ya Kuli ni vyema hivi sasa tutazame baadhi ya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na mwandishi wa riwaya hii kuwasilisha dhamira ya ukombozi. Hivyo, ufuatao ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti zinazohusiana na mbinu za kisanaa katika riwaya ya Kuli:

**Mbinu za Kisanaa katika Kuli**

Mbinu za kisanaa hurejelea ufundi wa kisanaa ambao hutumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa hadhira yake. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa mbinu za kisanaa ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia mwandishi katika kuijenga kazi yake ili iweze kueleweka vizuri kwa wasomaji au wasikilizaji wake na jamii kwa jumla. Ufundi huu wa kisanaa hutofautiana kutoka kwa mtunzi mmoja hadi mtunzi mwingine. Wamitila (2008) anaeleza kuwa, si jambo la ajabu kusikia msikilizaji au msomaji wa kazi ya fasihi akielezea kuwa amevutiwa sana na kazi fulani kuliko kazi fulani. Katika hali ya kawaida kinachomfanya msomaji kutoa kauli kama hiyo ni ule ufundi wa kisanaa ambao unawatofautisha waandishi wa kazi hizo mbili alizozisoma au kuzisikia.

Mwandishi Shafi Adam Shafi ni mmoja kati ya watunzi wa riwaya za Kiswahili anayesifika katika uandishi wa riwaya na kuheshimika sana kutokana na ufundi wa kisanaa alionao na kuutumia katika utunzi wa kazi zake. Mathalani, katika riwaya ya Kuli mwandishi ametumia mbinu mbalimbali za kisanaa katika kuwasilisha dhamira ya ukombozi kwa wasomaji wa riwaya hii. Miongozi mwa mbinu hizo za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi ni kama ifuatavyo:

**Matumizi ya Nyimbo katika Kuli**

Nyimbo ni kipera kilichopo katika utanzu wa ushairi na hivyo kutumiwa katika riwaya ya Kuli inaonesha kuwa ni sehemu ya ufundi wa kisanaa iliyotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha dhamira kwa wasomaji wake. Nyimbo huimbwa na kuburudisha pamoja na kufunza hadhira masuala ya muhimu na ya msingi katika
Maisha (Omary, 2015). Hii inatokana na ukweli kuwa ushairi ni utanzu mkongwe zaidi kuliko tanzu nyingine zote za fasihi ya Kiswahili. Kutokana na ukongwe wake ndio maana ni vigumu sana kuukosa ushairi katika harakati zozote zile za kufanikiwa katika maisha. Kwa mfano, hivi leo ili kiongozi wa kisiasa aweze kushinda uchaguzi ni lazima katika kampeni zake aambatane na wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva na taarabu. Nyimbo hizo huvuta wananchi katika kampeni na pia huwafanya wananchi kuwa watulivu na wasikilizaji wazuri wa sera za mgombea na kisha kuamua kumchagua au la.

Mwandishi Shafi Adam Shafi alifahamu kuwa akitumia nyimbo katika riwaya yake ya Kuli itawavutia zaidi

wasomaji wake na kutokana na kuvutiwa huko wataipata vizuri dhamira ya ukombozi. Hebu tuone mfano ufuatao:

*Kazi hiyo ngumu ilimalizika saa kumi na mbili Magharibi, na baada ya kumalizika kazi tu, Majaliwa hakusimama mpaka kwake. Alipofika nyumbani alimkuta Rashidi kachafuka, kelele nyumba nzima analia huku Bi Mashavu amempakata anachochea moto jikoni*

*Huku akimbembeleza: Usilie, usilie,*

*Ukiniliza na mie,*

*Machozi yako yaweke, Nikifa unililie*
*"Nini tena unamwacha mtoto analia tokea saa ile?" Majaliwa ambaye alikuwa chumbani akivua nguo aliuliza kwa hamaki. "Ah, hata sijui kinachomliza mtoto huyu," Bi Mashavu alisema. "Mnyonyeshe basi, labda ana njaa, Majaliwa aliamrisha. "Ntamnyonyesha vipi name n'na chungu jikoni?" Bi Mashavu alijibu akiwa naye kasha hamaki (uk.04).*

Katika dondoo lililopo hapo juu mwandishi ametumia wimbo ambao uliimbwa na Bi Mashavu kama bembelezi kwa mtoto Rashidi ambaye alikuwa akilia sana. Matumizi ya wimbo huu yametumiwa kama sehemu ya kutoa msisitizo wa kile ambacho mwandishi ametaka hadira yake ikipate. Nacho si kingine bali ni ukombozi wa Kijinsia ambapo tunamuona mwanamke akiwa ameelemewa na kazi nyingi za nyumbani tofauti na mwanaume ambaye hutoka asubuhi kwenda kazini na baade jioni hurejea nyumbani. Mwanamke akiamka asubuhi hana nafasi ya kupumzika mpaka saa y kulala inafika. Hili linadhihirika pale ambapo Bi Mashavu hakutaka kuacha kazi ya kupika eti kwa sababu mtoto analia bali alikuwa akifanya kazi ya kupika na kumbembeleza mtoto kwa pamoja ili asichelewe kutimiza majukumu yake.

Vilevile, katika dondoo hili tunaoneshwa kuwa mwanamke ni kiumbe anayempenda sana mwanae ndio maana Bi Mashavu hakumuacha mwanae akilia tu bila hata ya kumbembeleza. Hii inaonesha utayari wa mwanamke kubeba majukumu yake yote kwa pamoja bila ya kumwachia mtu. Hata hivyo, wanaume wengi huwa hawalioni suala hili na kujiona wao tu ndio wafanyao kazi na kazi kubwa ya mwanamke ni kula na kujipamba tu (Koda, 2000). Hili linathibitika pale ambapo Majaliwa anaonekana kumkaripia Bi Mashavu kuwa eti anamwacha mtoto analia tu bila kumjali.

Bila shaka huu ni mfumo dume na unapaswa ukomeshwe katika jamii kwa sababu unagandamiza mwanamke bila sababu za msingi. Mwandishi Shafi Adam Shafi ameutumia wimbo uliopo katika dondoo hapo juu kama kisisitizo cha kuonesha namna mwanamke alivyokuwa na majukumu mengi katika familia lakini bado watu wengi na hasa wanaume hawalitambui suala hili. Ukombozi wa kijinsia lazima uharakishwe katika jamii ili kuhakikisha kuwa mchango wa mwanamke katika maendeleo ya jamii na familia unatambulika na kuheshimika.
Baada ya kueleza juu ya matumizi ya mashairi kama mbinu ya kisanaa katika riwaya ya Kuli ni vyema hivi sasa tugeukie matumizi ya misemo na namna misemo hiyo inavyosaidia katika kuwasilisha dhamira ya ukombozi kwa hadhira ya riwaya hii.

**Matumizi ya Misemo katika Kuli**

Misemo ni kauli fupi fupi ambazo huwa na maneno yenye mafunzo na maadili ndani yake hasa pale inapotumiwa vizuri katika jamii. Tunasema pale inapotumiwa vizuri kutokana na ukweli kwamba ipo misemo ambayo hupotosha maadili na kufunza mambo maovu kwa jamii. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa misemo ni moja ya vipera vilivyopo katika utanzu wa semi ambao una historia ndefu sana katika maisha ya mwanadamu. Inasadikika kuwa utanzu wa semi ulianza sambamba na mwanadamu alipoanza kutumia lugha katika kuwasiliana.

Vipera vingine vya utanzu wa semi ni nahau, methali, vitendawili na simo. Semi ni utanzu wa fasihi ambao huibuka kila siku kutokana na maendeleo na shughuli mbalimbali za jamii. Semi huibuliwa kutokana na matukio yanayotokea kila siku katika jamii na hivyo, si makosa kusema kuwa misemo huzaliwa, hukuwa na hatime hufa ingawaje ipo misemo ambayo hudumu kwa kipindi kirefu katika maisha.

Mwandishi Shafi Adam Shafi ni miongoni mwa watunzi wa riwaya ya Kiswahili ambaye amekuwa msitari wa mbele katika kutumia misemo kama mbinu ya kisanaa katika kuwasilisha dhamira za ukombozi kwa jamii. Kwa mfano:

*Sikiliza Mzee Tindo, "Rashid alianza, "sisi siku nyingi tumefanya kazi pamoja na weye. Tunakuomba kama mzee wetu, sisi tunahisi*
*Kazi tunayoifanya ni kubwa na malipo tunayopata ni madogo basi tunahisi bora sasa tufanye utaratibu tuongezewe pesa." "Maneno aliyoyasema kijana huyu ni safi kabisa," Farjalla aliingilia kati… Mzee Tindo hakuwa na la kusema. Aliinamia chini kwa muda mdogo na baadae alinyanyua kicha chake na kumtazama Rashidi. Alimtazama kwa jicho la hamaki kwa kujua kwamba yote yale yalitokana nay eye, akaukumbuka ule usemi wa Kiswahili, "Kikulacho ki nguoni mwako".*

*Mzee Tindo alibaini kwa haraka kwamba wenzake wote wameazimu*

*Kikweli wala hapana mzaha (uk.49).*

Matumizi ya msemo "kikulacho ki nguoni mwako," katika dondoo lililopo hapo juu ni msemo uliotumiwa uonesha namna baadhi ya wananchi kutokuunga mkono harakati za ukombozi wa kisiasa, kijamii na kiuchumi katika jamii. Mzee Tindo alikuwa ni mtumishi wa bandarini ambaye alipata marupurupu mengi pamoja na upendeleo zaidi kutoka kwa matajiri na hususani tajiri mmoja aliyekuwa akimtumikia. Kutokana na hali hiyo aliona ni jambo sahihi kabisa wafanyakazi wenzake kuendelea kutumikishwa na kulipwa malipo kidogo. Pale ambapo wenzake wameona kwamba malipo hayatoshi na kuanza kudai malipo zaidi alitumia msemo wa "Kikulacho ki nguoni mwako," kujifariji na kutafakari namna ya kuhakikisha kuwa kiongozi wa madai ya kuongezewa malipo anafukuzwa kazi.

Kimsingi, matumizi ya msemo huu yanadhihirisha kwamba kudai haki na suala zima la kujikomboa kutoka katika mikono ya wanyonyaji ni wajibu wa kila mtu katika jamii. Kila mtu akifahamu kuwa huu ni wajibu wake basi itakuwa kazi nyepesi kuhakikisha kuwa haki na usawa vinapatikana katika jamii. Rashidi hakujali kuwa kwa kuwa Mzee Tindo ndiye aliyemsaidia akapata kazi basi asidai haki ya malipo mazuri kwa kumhofia Mzee Tindo. Kijana Rashidi alisimama kidete katika kudai
Haki ya malipo mazuri yanayolingana na ugumu wa kazi pamoja na faida anayoipata bosi wa kazi hiyo. Katika jamii ya leo watu kama hao wapo na hutumia nguvu zao

na akili zao zote kuhakikisha kuwa harakati za ukombozi kutokana na unyonyaji unaofanywa na baadhi ya watu mahali pa kazi haufanikiwi. Watu kama hao hawapaswi kupewa nafasi bali wanatakiwa wapingwe kwa nguvu zote ili kusaidia kuifanya dunia kuwa yenye haki na usawa kwa watu wote.

Baada ya kutoa maelezo juu ya matumizi ya misemo katika riwaya ya Kuli na kuonesha ni kwa vipi msemo uliotumika katika riwaya hii unasisitiza azma ya ukombozi wa kifikra na kiuchumi katika jamii sasa tunahamia katika matumizi ya takriri.

**Matumizi ya Takriri katika Kuli**

Takriri ni marudiorudio yanayofanywa na mwandishi katika kazi yake ya fasihi akiwa na sababu maalumu na kubwa ikiwa ni kutoa msisitizo wa kile anachokielezea au kile anachotaka hadhira yake ikipate. Marudiorudio au takriri hujitokeza kwa namna mbalimbali kiwa ni pamoja takriri silabi ambapo silabi fulani hurudiwa zaidi kuliko silabi nyingine na takriri neno ambapo neno fulani hujitokeza mara nyingi kuliko maneno mengine. Pia kuna takriri sentensi na takriri aya ambapo sentensi au aya nzima hurudiwa zaidi ya mara moja.

Lengo kuu la kufanya marudiorudio ni kutoa msisitizo au kuonesha uziti wa jambo fulani ambalo mwandishi anataka hadhira yake ilizingatie. Takriri ni kipengele cha kisanaa ambacho kina asili yake katika fasihi simulizi lakini hivi sasa kinatumika pia katika fasihi Andishi. Mwandishi Shafi Adam Shafi ametumia takriri katika katika riwaya ya Kuli lengo likiwa ni kutoa msisitizo wa dhamira ya ukombozi wa kifikra, kiuchumi, kijamii na kijinsia. Mathalani katika kutoa msisitizo wa ukombozi wa kiuchumi, mwandishi anasema:

*Simile! Simile!" Mmoja wao alitangulia mbele akipiga kelele kuwatahadharisha wapiti njia na wengine walilisukuma rikwama lililojaa magunia ya karafuu mbio wakielekea Malindi. Kama kawaida mshika usukani alikuwa Mzee Tindo (uk.38).*

Katika dondoo hili kuna matumizi ya takriri neno ambapo neno "simile," limerudiwa mara mbili. Neno hili limerudiwa kwa kunia ya kutoa msisitizo juu ya shughuli ya ukombozi wa kiuchumi ambapo Rashidi pamoja na wenzake wanabeba mizingo bandarini ili kuweza kujipatia kipato cha kujikimu kimaisha. Hivyo, kwa kutumia takriri ya neno hili watu walioko barabarani huwapisha akina Mzee Tindo na rikwama lao na hatimaye kufanikisha kazi ya siku na kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yao na hivyo kujikwamua kiuchumi. Kazi ya kujituma waliyokuwa wakiifanya akina Rashidi na wenzake ni mfano mzuri wa kuigwa na watu wote katika jamii kwa kuwa kujituma ndio msingi wa mafanikio. Haijalishi kwamba malipo ya kazi ni kiasi gani lakini mtu anafanya kazi kwanza na kupata kipato kidogo ndipo baadae aweze kupata kikubwa zaidi.

**Matumizi ya Barua**

Barua ni chombo cha kupeana habari au taarifa fulani kuhusu jambo rasmi au la kirafiki na kijamii. Barua huandikwa na mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine kwa maandishi ya mkono au yaliyochapwa. Watunzi wa kazi za fasihi kama Shafi Adam

Shafi hutumia barua kama mbinu ya kisanaa ili kufikisha ujumbe uliopo katika

Riwaya zake. Katika riwaya ya Kuli kuna matumizi ya barua kama ifuatavyo:

*Kwa mume wangu mpenzi,*

*Nina wingi wa masikitiko kwa yaliyokufika na nakuombea kila la heri. Hali ya maisha ni kama unavyojua. Nimepata habari kwamba wenzako hawakufanikiwa lakini watazidi kuendelea na juhudi zao mpaka wajue moja. Nilielezwa kwa kirefu kuhusu matatizo yenu na sasa nimefahamu kazi muhimu uliyokuwa nayo na kusababisha uchelewe kurudi nyumbani nyakati za usiku. Nakuhakikishia mume wangu kwamba pindi ukijaaliwa kutoka sitolalamika tena wala sitokawia kukufungulia mlango pindi utakaporudi saa sita au saba za usiku.*

*Nimesikia kwamba, hukumu yako itakuwa siku ya Ijumaa na siku hiyo nitajiburura hivyohivyo na tumbo langu nije mahakamani. Sina mengi ila nakutakia kila la kheri na mafanikio. Amina.*
*Wako wa milele,*
*(Uk. 197-198).*

Barua hii iliandikwa na mke wa Rashidi aliyefahamika kwa jina la Amina ambaye alionyesha kumtia moyo mume wake katika harakati za kujiletea ukombozi. Mkewe alimuahidi kwamba kamwe hawezi kulalamika tena kutokana na mumewe kurudi nyumbani akiwa amechelewa hasa nyakati za usiku. Hii ni baada ya kutambua kwamba mumewe hakuwa akichelewa kwa makusudi bali alikuwa na kazi ngumu ya kufanya. Matumizi ya barua hii yamekuwa ni mbinu za kisanaa ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira pale tu msomaji anapokutana na barua hii hulazimika kuisoma kwa makini ili kuelewa ni kitu gani kinachozungumzwa ndani ya barua hii. Matumizi ya mbinu kama hii yanatokana na ubunifu wa hali ya juu alio nao mwandishi.

**Matumizi ya Jina la Kitabu**

Jina la kitabu hutumiwa kama mbinu ya kisanaa pale ambapo jina la kitabu husika linapokuwa linasawiri na kuakisi mambo yanayowasilishwa ndani ya kitabu. Baadhi

Ya watunzi wa kazi za fasihi huteua jina la kitabu ambalo kwa namna moja au nyingine hufumbata visa na matukio ndani ya riwaya. Mwandishi wa riwaya ya Kuli ameitumia mbinu hii kwa ubunifu kwani jina la kitabu Kuli linaendana moja kwa moja na visa na matukio yayofanywa au kuwakumba makuli ambao ni watumishi wa kubeba mizigo bandarini.

Kimsingi, Kuli ni mtumishi ambaye amekuwa hathaminiwi hata kidogo na mwajiri wake ndio maana amekuwa akilipwa ujira kidogo na akipata madhara ya ajali kutokana na kazi yake hakuna msaada wowote anaopatiwa. Kuli ambaye anaonekana kuwa ni kimbelembele katika kudai haki hufungwa gerezani kama ilivyokuwa kwa Rashidi. Hii inaonyesha kuwa jina la kitabu Kuli limesawiri hali halisi ya maisha ya mfanyakazi wa kubeba mizigo bandarini anayefahamika kama Kuli.

**Hitimisho**

Katika sura hii tumewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti wetu kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Miongoni mwa yaliyowasilishwa katika sura hii ni pamoja ukombozi wa kifikra, ukombozi wa kijamii, ukombozi wa kijinsia na ukombozi wa kiuchumi. Sambamba na dhamira hizi za ukombozi zilizowasilishwa pia tumewasilisha mbinu za kisanaa kama vile matumizi ya nyimbo, misemo, takriri, barua na jina la kitabu. Sura inayofuata inawasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo kwa ajili ya utafiti zaidi.

**Marejeo**

Abdallah, A.O. (2014), "Kuchunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya za Shafi Adam Shafi: Mifano wa Kuli na Vuta N'kuvuta" Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Doris,Ken na Norah.(2016). "Kielezi cha Marudio ya Kiswahili: Nairubi; Mentor Publishing Co.Ltd.

Khamis, S.A.M.(2007),"Utandawazi au Utandawizi ?Jinsi lugha riwaya mpya ya Kiswahili inavyodaia", katika Kiswahili, juzuu namba 70, Dar es Salaam: TUKI, Ku.47-66.

Lyabwene M. Mtahabwa (2020)," Tuheshimu Tamaduni Zetu na za Wengine Kitabu cha Ziada, Darasa la Tatu na Nne" Taasisi ya Elimu Tanzania, Dar es Salaam.

Njuguna, H. (2015). "Ukiushi katika Ushairi wa Amri Abedi na Kithaka wa Mberia" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Omary,M. (2015), " Kuchunguza ufasihi simulizi katika kazi za Euphrase Kezilahabi: Mfano wa Vitabu vya Kichomi, Karibu Ndani Dhifa" Tasnifu ya Uzamivu, Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Okal,B.O. (2021). "Uhakiki wa Riwaya ya Paradiso kwa Msingi wa Nadharia ya Uhalisi" Katika Swahili Forum 28. Uk,14-33.

Ramadhani,S.K. (2013), "Usawiri wa mwanamke katika tarabu ya mipasho: Mfano kutoka nyimbo za Mzee Yussuf Mzee". Tasinifu ya M.A Kiswahili, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.